

**HOTUBA YA MHE: ENG. STELLA MARTIN MANYANYA (MB) MKUU WA MKOA WA RUKWA ALIYOITOYA KWENYE KIKAO KAZI CHA KUJADILI MIKAKATI YA KUPUNGUZA VIFO VYA WAJAWAZITO, HALI YA HUDUMA ZA CHF/NHIF NA MAENDELEO YA WANANCHI MKOANI RUKWA KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MANISPAA YA SUMBAWANGA TAREHE 13 SEPTEMBA, 2014**

Katibu Tawala Mkoa,

Waheshimiwa wa Wakuu wa Wilaya,

Mganga Mkuu wa Mkoa,

Makatibu Tawala Wasaidizi

Wakurugenzi wa Halmashauri.

Viongozi na Watendaji wa Serikali,

Mabibi na Mabwana,

### **Habari ya Asubuhi**

Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutuwezesha sisi sote kukutana mahali hapa siku hii ya leo

Pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwawezesha ninyi nyote mnaotoka nje ya Manispaa ya Sumbawanga kusafiri salama na kuweza kuhudhuria Kikao hiki. Ni wazi kila mmoja wetu anatambua na ameshuhudia kupitia Vyombo vya Habari, matukio mfululizo ya Ajali za Barabarani kwa siku za hivi karibu.

Aidha napenda pia kuwashukuruni nyote kwa kuitikia wito huu wa Kikao hiki, ambacho tutapata fursa ya kuitizama Sekta ya Afya katika Mkoa wetu kwa mapana yake na kukumbushana Wajibu wetu kama Watendaji ambao Mkoa na Taifa kwa ujumla inatutegemea.

Kikao hiki ni muhimu sana katika kuweka mikakati ya pamoja na kuitekeleza ili tuweze kuongea lugha moja “Afya na Ustawi wa Wananchi wetu”.

Kikao kazi hiki ni fursa muhimu sana kwa sisi sote kuweza kupeana uzoefu na kuona maeneo gani yanahitaji nguvu ya ziada na maeneo gani tumefanya vizuri ili tuweze ku “maintain”

Hali ya utoaji wa huduma katika Sekta ya Afya katika vituo vyetu imeendelea kuimariika hasa baada ya serikali kuongeza vituo kwa mpango wa MMAM, na upatikanaji wa vifaa tiba na watumishi pamoja na kuongezeka kwa uelewa wa wananchi juu ya umuhimu wa tiba na kujikinga na maradhi.

Hali ya magojwa na vifo imeendelea kupungua mwaka hadi mwaka na Mkoo unaendelea kusisitiza Elimu ya kinga iongezwe ili kupunguza gharama za Matibabu ambazo zimeendelea kupanda sambamba na mabadiliko ya uchumi.

Katika magonjwa Kumi ambayo yanawakabili Wananchi wetu ndani ya Mkoo, mengi yanazuilika kinachotakiwa ni kuongeza ufahamu na jinsi ya kujikinga . Magojwa hayo ni kama yafuatayo:-

- Malaria
- Upungufu wa Damu
- Kuharisha
- Homa ya mapafu
- Neumonia
- Utapiamlo
- Kuungua
- Magonjwa ya njia ya mkojo
- Kuvunjika

Magojwa haya yanaweza kuzuilika kwa kufuata njia sahihi za kujikinga.

Hali ya Afya ya Mama na Mtoto (au Uzazi) nayo imeendelea kuimarika. Mkao umeendelea kushuhudia kupungua kila mwaka kwa vifo vinavyosababishwa na Uzazi toka 177/100,000 (2010) hadi 131/100,000 (2013). Japokuwa idadi ya vifo vimepungua kwa tarakimu kuna haja ya kuongeza bidii katika eneo hilo kwa kila mmoja wetu kutimiza wajibu wake ili kuokoa Maisha ya Mama zetu ambao wanafariki wakiwa wanaleta uhai duniani.

Mkao uko chini ya lengo la kitaifa la vifo 193/100,000 kushuka kwa vifo hivi ni juhudzi zinazofanywa na Mkao kwa kushirikiana na Halmashauri zake pamoja na wadau mbalimbali wa Maendeleo. Hata hivyo bado tunashuhudia vifo vikitokea ambavyo vinaweza kabisa kuzuilika.

Baadhi ya changamoto zinazosababisha Vifo hivi vyatia wajawazito:-

- Kuchelewesha wajawazito kufika vituo vyatia kutolea huduma.
- Wajawazito wengi kujifungulia nyumbani au kwa wakunga wa jadi (42%).
- Mahudhurio yasiyordhisha kwenye kliniki za wajawazito - 40% (hudhurio la 4).
- Kutozingatia uzazi wa mpango ( wastani wa 5.4).
- Wajawazito kutumia dawa za asili za kuongeza uchungu wakati wa kujifungua na kusababisha vizazi kufumuka/ kupasuka.
- Mama wajawazito kufanyishwa shughuli ngumu na nyingi bila kuzingatia afya zao.

Hizo ni baadhi tu ya changamoto zinazosababisha kuendelea kuwapo kwa vifo vinavyotokana na Uzazi.

Kutokana na kuimarika kwa huduma za Afya katika Mkao wetu, ni kwa baadhi ya maeneo tu Wananchi wanalazimika kutembea umbali mrefu kwa ajili ya kufuata huduma za Afya. Ni dhahiri kabisa kuwa kwa kutumia fursa hiyo vizuri tunaweza kupunguza na kuzuia vifo vyatia zaidi.

Pia Mkao kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo umeongeza na unaendelea kuongeza idadi ya Vyumba Vya Upasuaji

(Theatres). Kwamwaka 2013/2014 tumeongeza vyumba vyua upasuaji

Wampembe na Mtowisa na vimeanza kufanya kazi. Ni jukumu letu kuwawahisha wajawazito kliniki ili wakapate huduma mapema na pale inapoonekana wana matatizo ya kujifungua wapelekwe haraka kwenye vituo hivi vyenye huduma ya upasuaji.

Kwa niaba ya Serikali ya Mkoa na Wananchi wote kwa ujumla tunaendele kuwashukuru sana Wadau Maendeleo hawa waliosaidia kupatikana kwa vyumba hivi vyua upasuaji. Pia tunaomba wananchi tushirikiane wote kuimarisha upatikanaji wa majengo ya kutosha kutolea huduma hasa upasuaji katika maeneo yetu kwa kujitolea michango ya hali na mali.

Napenda kuziagiza Halmashauri zote za Mkoa, wahakikishe vyumba nane (8) vyua Upasuaji vinavyoendelea kujengwa vinakamilika mapema na kuanza kutoa huduma.

Napenda kutumia fursa hii pia kuzungumzia ugonjwa wa Ebola. Mkoa wetu unapakana na Nchi ya Congo DRC ambayo kwa sasa kuna mlipuko wa ugonjwa wa Ebola. Ugonjwa huu ni hatari sana hadi sasa ni takribani Watu 33 wamesha fariki dunia kutokana na Ebola

Ebola ni ugonjwa unaoenea kwa kasi ya ajabu na unaweza kusababisha vifo hadi 70% ya wagojwa. Kutokana na mwingiliano uliopo baina yetu na wenzetu wa Congo DRC hasa kwenye masuala ya biashara na matibabu, na mambo mengine ya kijamii, tunatakiwa kuwa katika hali ya tahadhari kwa kila mmoja wetu kuwa mlinzi na kubaini wanaoingia kinyume na taratibu waweze kudhibitiwa, na endapo kuna mtu mwenye dalili za ugonjwa huo taarifa itolewe haraka katika Vituo vyua Afya kwa hatua za haraka.

Hadi sasa Mkao umeshachukua hatua mbalimbali za kupambana na Ugonjwa huu. Hata hivyo tunahitaji kusisitiza zaidi kuhusu kujikinga hasa yale maeneo yenyewe mwingiliano mkubwa.

Serikali yetu inaendelea na jitihada za kuhakikisha huduma za Afya zinawafikia wananchi wote. Ili kutimiza lengo hilo nguvu za wananchi nazo zinahitajika. Tunawashukuru sana wananchi kwa kuitikia wito wa kuchangia nguvu kwenye mpango wa MMAM. Ili tuweze kupata huduma nzuri, vituo vinatakiwa kuwa na dawa na vifaa tiba vyatutorsha.

Bajeti ya dawa inayotolewa na serikali inaendelea kupungua mwaka hadi mwaka , ili kukabiliana na upungufu huo tuendelee kuhamasisha Wananchi wajunge na mpango wa CHF, ili kuimarisha upatikanaji wa dawa katika vituo vyetu. Fedha zote za CHF zinatumika kwenye kituo husika, hivyo kamati za vituo zihakikishe michango hii inatumika ipasavyo na juhudzi zinaongezwa kuhakikisha uchangiaji wa mfuko unaongezeka tutoke kwenye asilimia 8% ya sasa,

Tumeitana leo kujaribu kuangalia ni jinsi gani tunatoka hapo tulipo. Tunatakiwa kuhakikisha tunatoka kwenye vifo vyatutorsha wajawazito toka 138/100,000 hadi 90/100,000 japokuwa kifo cha mjamzito hakikubaliki

- Watoto wachanga – 3.3/1000 hadi 2/1000.
- Watoto chini ya miaka 5 – 48/1000 hadi /40/1000.
- Kuongeza makusanyo ya CHF toka 8% hadi 100%
- Tunahakikisha wajawazito wote wanahuduria kliniki na kujifungulia kliniki.
- Wananchi wanapata Elimu na huduma ya kupanga uzazi.

- Wakunga wa jadi wanasaidia wajawazito kujifungulia kwenye vituo vya huduma.
- Wananchi wanajikinga dhidi ya Ebola na kutoa taarifa mapema wanapoona kuna mtu mwenye dalili za Ebola.
- Ushiriki wa wananchi kwenye shughuli za maendeleo.

Afya ya mama mjamzito, mtoto mchanga na jamii yote kwa ujumla ni kazi yetu sisi wote. Tuhakikishe wananchi wetu wote wanapata huduma zinazowasaidia kuimarisha Afya zao.

Tukiunganisha nguvu zetu wote tutapunguza kama siyo kuondoa kabisa vifo vinavyoweza kuzuilika.

Mwisho napenda kuongelea kuhusu suala la Kongamano la Uwekezaji lililo mbele yetu ambalo litafanyika tarehe 26 Oktoba, 2014 sambamba na maadhimisho ya Miaka 40 ya Mkoa wa Rukwa.

Kila mmoja wetu awe balozi wa kuitangaza siku hiyo na kushiriki ili shughuli yetu iweze kufana. Kipaumbele kinatolewa kwa Wawekezaji wa ndani ya Mkoa, wekezeni katika ujenzi wa Nyumba za Kisasa za kuishi pamoja na Hoteli, katika maeneo hayo wengi wetu tunaweza kuwekeza mahitaji ni mengi, kadri Mkoa unavyozidi kufunguka ndivyo ambavyo uhitaji wa makazi unavyoongezeka.

Asanteni kwa kunisikiliza kikao kimefunguliwa rasmi.

Mhe: Eng. Stella Martin Manyanya (Mb)

**MKUU WA MKOA WA RUKWA**